

Learning by Ear 2011 – Road Safety

Episode 08 – Don't drink and drive

Text: Victoria Averill

Editing: Johannes Beck, Katrin Ogunsade

Proofreading: Martin Vogl

CHARACTERS:

Onyesho la 1:

- ♣ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)
- ♣ NANCY (MSICHANA, UMRI WA MIAKA13, rafiki yake Alice)

Onyesho la 2:

- ♣ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)
- ♣ PAMELA (MWANAMKE, UMRI WA 30-40)

Onyesho la 3:

- ♣ NANCY (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)
- ♣ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)
- ♣ DOUGLAS (MVULANA, UMRI WA MIAKA 18, kaka yake Nancy)

Onyesho la 4:

- ♣ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)
- ♣ NANCY (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)

♣ DOUGLAS (MVULANA, UMRI WA MIAKA 18)

Onyesho la 5:

♣ ALICE (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)

♣ NANCY (MSICHANA, UMRI WA MIAKA 13)

♣ DOUGLAS (MVULANA, UMRI WA MIAKA 18)

Onyesho la 6:

♣ MSOMAJI HABARI (MWANAMUME AU MWANAMKE)

Intro/Studio/Outro:

♣ MTANGAZAJI BEATRICE (MWANAMKE)

♣ GEORGE – MTAALAMU WA USALAMA BARABARANI
(MWANAMUME)

Intro:

1. Beatrice: Karibu kwenye makala ya Noa Bongo Jenga Maisha yako na mchezo wetu wa redio kuhusu usalama barabarani. Jina langu ni Beatrice. Kwenye vipindi vyetu vyote kumi tunaandamana na familia ya Wanjiru. Tunaangazia maisha yao ambapo walishuhudia maafa yanayotokana na ukosefu wa usalama barabarani barani Afrika. Nitazungumza pia na mtaalamu wa usalama barabarani ili tujue jinsi ya kuhakikisha usalama zaidi barabarani kwa lengo la kuokoa maisha. Katika kipindi hiki, Alice na rafiki yake Nancy wamefunga shule. Wanaamua kwenda kusherehekea. Hata hivyo hawatilii maanani hatari ya mtu kuendesha gari akiwa mlevi. Endelea kuwa nasi usikilize kisa hiki cha siku iliyoanza na furaha ikaishia na masaibu!

Scene One: leaving school

2. SFX Atmo: school bell, children chattering, laughing

3. ALICE: Hakuna kwenda shule kwa miezi miwili... raha iliyoje!
Na sote tumepita mitihani yetu, hata na wewe Nancy, umepita hisabati! Bila shaka ni kutokana msaada wangu. Unafaa kuninunulia soda!

4. NANCY: Achana na soda, leo usiku twende tukasherehekee!
Ndugu yangu amefaulu mtihani wake wa udereva, baba atamruhusu kuendesha gari lake na anaweza pia kutununulia vileo kidogo maana umri wake unamruhusu. Waonaje?

5. ALICE: Wazo zuri! Babako kweli atamruhusu kuendesha gari ingawa kafaulu hivi karibuni? Natumai hatakunywa pombe kisha aendeshe gari?

6. NANCY: Naam, baba hana tatizo. Na kusema kweli Douglas hanywi pombe. Anapenda kuvuta kiasi. **(secretly)** Yaani bangi... lakini bangi haikuathiri vyovyote. Sawa, tutaonana baadaye, tukupitie kama saa moja hivi?

7. ALICE: Sawa. Tutaonana halafu!

Scene Two: Alice's house

8. SFX Atmo: living room, cooking

9. ALICE: Mama, waonaje nguo hii?

10. PAMELA: Naam mwanangu. Inakupendeza. Umesema unakwenda wapi?

11. ALICE: Hata sijui wapi, lakini mjini. Nancy na kaka yake watanipitia. Kisha tutaungana na marafiki zetu wengine mjini ... Sidhani kama tutachelewa kurudi.

12. PAMELA: Sawa, lakini muwe waangalifu. Na kaka yake Nancy kweli anaweza kuendesha gari vizuri? Ameshapita mtihani wake wa udereva na kupata uzoefu mwingi wa kushika usukani?

13. SFX: Car hooting

14. ALICE: Ndio hao. Usiwe na wasiwasi mama, tutaonana baadaye.

15. SFX: Slamming of door

16. PAMELA: (shouting) Kwaheri Alice, na muwe waangalifu!

Scene 3: driving in the car

17. SFX Atmo: driving along

18. NANCY: Raha iliyoje kujiendeshea gari na kuwa huru!

19. ALICE: Naam. Raha kweli. Unavuta nini Douglas?

20. DOUGLAS: Aah, hashishi kidogo, yaani bangi ... Unataka kidogo?

21. ALICE: Aha, hapana. Na inafaa kuvuta hicho kitu huku ukiendesha gari?

22. DOUGLAS: Hakuna shida! Inanimakinisha ninapoendesha gari. Sina papara kama madereva hawa wengine wote wapumbavu wanaoendesha magari barabarani.

23. NANCY: Usiwe na hofu Alice. Onja pombe kidogo. Douglas ametununulia. Kunywa kidogo ujifurahishe nawe. Si tumekuja leo usiku kusherehekea?

24. ALICE: Sawa. Asante.

25. NANCY: Tujifurahishe! Tusherehekee kwa kufunga shule na kupata fursa ya kujifurahisha!

26. SFX: **clinking bottles**

27. NANCY: Tazama pale, naona kama Fred ... Anaingia kwenye
baa. Tumuwahi. **(honk and shouting)** Fred, tungonjee!
Tutaegesha gari kisha tutajiunga nawe kwenye baa.

Scene Four – outside the bar

28. SFX Atmo: **cars going past, people singing, people drinking**

29. ALICE: **(tired)** Nancy, najisikia mchovu. Tunaweza kurudi
nyumbani sasa?

30. NANCY: **(slurring words)** Ati? Mara moja hii? Mapema sana .

31. ALICE: Si mapema, Nancy. Ni saa saba usiku na tayari
tumekuweko hapa kwa muda wa saa sita. Ninahitaji
kwenda kula. Sijisikii vizuri

- 32. NANCY:** Sawa, ebu nimtafute Douglas. Nawe mtafute Fred ili naye pia tumpeleke nyumbani kwao.
- 33. ALICE:** Nimemtafuta. Mwenye baa anasema Fred amelewa chakari na ametoka nje kwenye kupunga upepo na pia kujilaza. Lakini sijui kenda wapi.
- 34. NANCY:** Ajabu. Huyu hapa Douglas kwa hivyo tuingie sote kwenye gari kisha tuzunguke tumtafute Fred...Douglas una nini?
- 35. DOUGLAS:** **(talking in a slow manner)** eehe, sawa. Gari liko wapi?
- 36. ALICE:** Aah... Nadhani tumelipita. Kwani hukumbuki ulikoliegesha?
- 37. DOUGLAS:** Ninakumbuka! Nadhani nililiegesha pale. Au pengine... **(surprised)** Hapana, ni hapa! Njooni! Tuingie kwenye gari tumtafute Fred.

38. SFX: Car doors opening and closing. Motor starting.

Scene Five – on the road searching for Fred

39. SFX Atmo: Inside the car, driving, car motor sounds

40. NANCY: Douglas, ebu endesha polepole tulizunguke hili jumba huenda tukamwona Fred. Nasikia ameondoka kwenye baa kwenda kupunga upepo na kupumzika.

41. DOUGLAS: Sawa, ukimuona nijulisha.

42. SFX: Bump sound, car ran over something

43. ALICE: Ebu simama! Nini hicho? Nadhani umekanyaga kitu.

44. DOUGLAS: Tulia nawe Alice. Nadhani ni tuta la barabarani, yale matuta ya kuzuia magari kwenda kasi.

- 45. ALICE:** Hakuna matuta katika barabara hii. Douglas simamisha gari. Umekanyaga kitu fulani.
- 46. NANCY:** Pengine ni mbwa. Ebu nishuke nione ni nini!
- 47. SFX:** **Car engine off**
- 48. SFX:** **Car door opens from inside**
- 49. NANCY:** **(Nancy gets out of the car, walks a couple of meters)**
(Screams) Hapana! Hapana!!!
- 50. ALICE:** **(still inside the car)** Nancy, kuna nini?
- 51. NANCY:** Mungu wangu. Ni Fred. Amepigwa dafrau. **(desperate)**
Alice nisaidie! Tafadhali, Alice, nisaidie!
- 52. SFX:** **Car door opens**

53. ALICE: **(Alice gets out of the car and walks to Nancy)** Mungu wangu! Nancy, bado anapumua? Tumempiga dafrau. Douglas, tafuta msaada! Ni lazima tumpeleke hospitalini!

54. DOUGLAS: **(approaching Nancy and Alice, drunk and shocked)**
Kweli ni Fred... Anavuja damu... **(losing control, panicking)** Tusaidieni jamani! Tumsaidie!

55. SFX: **Police sirens**

56. ALICE: Polisi wanakuja. Tunahitaji ambalesi kumsaidia Fred. Tusaidieni, Tafadhalini tusaidieni!

Scene Six – radio broadcast

57. SFX: **beeps for 9 o'clock news on the radio**

58. NEWSREADER: Hamjambo na karibuni kwenye habari zetu za saa tatu: Vijana watatu wametiwa nguvuni baada ya gari lao kumpiga dafrau na kumuua mvulana mmoja jana usiku. Kwa mujibu wa polisi, vijana hao walikuwa wakiendesha gari wakiwa walevi. Dereva wa gari hilo ameshtakiwa kwa kosa la kuuu bila kukusudia. Iwapo atapatikana na hatia, huenda akakabiliwa na kifungo cha miaka isiyozidi minane gerezani. Vijana wengine wawili waliokuwa wamekamatwa wameachilia kwa dhamana baada ya kuhojiwa na huenda wakatozwa faini isiyozidi ... **(fade out)**...dola elfu moja fedha za Marekani. Mvulana aliyepigwa dafrau alikuwa alikuwa na umri wa miaka 15. Kulingana na msemaji wa polisi vijana wote hao walikuwa marafiki na walikuwa wakisherehekea kwa kufunga shule mwisho wa muhula

END OF SCENE FIVE

SHORT MUSIC 59. BEATRICE: Karibuni tena. Pamoja nami studiosi

Formatiert: Block

Gelöscht: ¶

hivi sasa huyu hapa George, mtaalamu wetu wa
usalama barabarani. Karibu George!

60. GEORGE: Asante sana.

61. BEATRICE: Naam, George, Usiku ulioanzia na furaha umeishia
kuwa na msiba...

62. GEORGE: Naam, Beatrice, inasikitisha. Hata hivyo hatma hii ya
mambo ina lengo la kusesitiza hatari iliyopo kwa
kuendesha gari mtu akiwa mlevi au akiwa anatumia
mihadarati. Pombe na mihadarati kama vile bangi
humtatiza mtu akakosa kumakinika. Huwa si mwepesi
wa kutenda mambo na hata hana uwezo mkubwa wa
kufikiri kwa kasi. Douglas alidhani kwamba amevuka
tuta la barabarani lakini kumbe amempiga mtu dafrau!

63. BEATRICE: Na je hili tatizo la kuendesha magari watu wakiwa walevi ni kubwa barani Afrika?

64. GEORGE: Naam, ni kubwa. Katika mataifa mengi barani Afrika polisi hawawaadhibu watu wanaopatika wakiendesha magari wakiwa walevi. Huwaachilia huru vivi hivi tu bila kushtakiwa au wakishatoa hongo. Lakini ukisababisha kifo cha mtu, kama alivyofanya Douglas, au umjeruhi mtu, utabaki na athari hiyo maisha yako yote. Huenda Douglas akasukumwa gerezani kwa miaka kadha.

Gelöscht: ¶

65. BEATRICE: Tuseme usiku mmoja tu wa kwenda ulevini na kisha kuendesha gari unaweza kuingiza kisirani kwenye maisha yako?

66. GEORGE: Ndiyo hivyo. Amejiharibia maisha yake pamoja na maisha ya familia ya mvulana aliyefariki. Hatakuwa tena kama alivyokuwa zamani. Kwa hivyo ni muhimu kuzingatia hatari ya kuendesha gari mtu akiwa mlevi.

67. BEATRICE: Na je ni sawa mtu anywe chupa moja ya bia kisha Aendeshe gari?

68. GEORGE: Hata baada ya chupa moja mtu huwa tena si mwepesi wa kufikiria. Kwa hivyo hata kama mtu haleweshwi na chupa moja ya bia, ni bora zaidi kutokunywa pombe iwapo unaendesha gari. Ni rahisi zaidi kwa mtu mlevi kusababisha ajali. Kimsingi: Ukinywa pombe usiendeshe gari.

69. BEATRICE: Asante sana George.

MUSIC (FADE UNDER OUTRO)

OUTRO

70. BEATRICE: Katika kipindi kitakachofuata itakuwa zamu ya Nelson kutumia vizuri barabara atakapokuwa akiendesha baiskeli yake. Tunatumai umefurahi na kujifunza mengi kutokana na mchezo wetu wa redio ulioandikwa na Victoria Averill.

Ukitaka kusikiliza kipindi hiki kwa mara nyingine, basi tazama wavuti wetu www.dw.de/lbe. Asante sana kwa kujiunga nasi na jitahidi kuweka usalama barabarani!